# KATIBA

# YA

# CHAMA CHA MPIRA WA KIKAPU MKOA WA XXXXXXXX

# XXXXXX REGIONAL BASKETBALL ASSOCIATION

## TOLEO LA KWANZA

## 2021

# YALIYOMO


SURA YA KWANZA ..... 1
JINA, MAKAZI, TAFSIRI, MADHUMUNI NA WAJIBU ..... 1
IBARA 1 ..... 1
JINA ..... 1
IBARA 2 ..... 1
MAKAZI ..... 1
IBARA 3 ..... 1
MATUMIZI ..... 1
IBARA YA 4 ..... 1
TAFSIRI ..... 1
IBARA YA 5 ..... 1
A: MADHUMUNI YA KUUNDA CHAMA ..... 1
SURA YA PILI ..... 2
IBARA 6 ..... 2
UANACHAMA ..... 2
IBARA YA 7 ..... 3
KIINGILIO NA ADA YA UANACHAMA ..... 3
IBARA YA 8 ..... 3
HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA ..... 3
IBARA YA 9 ..... 3
UKOMO NA KUPOTEZA UANACHAMA ..... 3
IBARA YA 10 ..... 3
KURUDISHIWA UANACHAMA ..... 3
SURA YA TATU ..... 4
IBARA YA 11 ..... 4
MUUNDO WA UONGOZI, SIFA, KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA CHAMA ..... 4
IBARA YA 12 ..... 4
MUDA WA UONGOZI ..... 4
IBARA YA 13 ..... 4
KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA CHAMA ..... 4
SURA YA NNE ..... 6
IBARA YA 14 ..... 6
MIKUTANO MBALIMBALI YA CHAMA CHA MPIRA WA KIKAPU ..... 6
SURA YA TANO ..... 8
IBARA YA 15 ..... 8
VYANZO VYA MAPATO, UTUNZAJI NA MATUMIZI YA FEDHA YA CHAMA ..... 8
SURA YA SITA ..... 9
IBARA YA 16 ..... 9
KUTOFANYIKA KWA UCHAGUZI, MIGOGORO, MAREKEBISHO YA KATIBA, AKIDI, KUVUNJIKA KWA CHAMA ..... 9

# SURA YA KWANZA

## JINA, MAKAZI, TAFSIRI, MADHUMUNI NA WAJIBU

### IBARA 1

### JINA

Jina la Chama cha Mpira wa kikapu mkoa wa XXXXXXX litakuwa: **CHAMA CHA MPIRA WA KIKAPU MKOA WA XXXXXXXX** (**XXXXXX REGIONAL BASKETBALL ASSOCIATION)**

### IBARA 2

### MAKAZI

Makao Makuu ya Klabu ya Michezo yatakuwa **XXXXX MJINI** na yanapatikana kwa anuani ya **S.L.P PPPP XXXXXX TANZANIA**

### IBARA 3

### MATUMIZI

Katiba hii itatumiwa na wanachama na kuendesha shughuli zote zinazosimamia Mpira wa Kikapu katika Mkoa wa XXXXX na Katiba za Wanachama kutoka katika Klabu au Timu hazitakuwa zinapingana na Katiba hii.

### IBARA YA 4

### TAFSIRI

i) **BMT** Baraza la Michezo Taifa
i) **BODI** ni chombo cha utawala katika Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania
ii) **BODI YA WADHAMINI** ni kikundi cha watu waliojitoa kwa hiari kudhamini chama ikiwemo fedha, mali na miradi au shughuli nyingine za Chama
iii) **CHAMA** ni muunganiko wa watu waliokusanyika sehemu moja wenye nia ya kushiriki shughuli fulani au mchezo fulani kwa pamoja
iv) **KATIBA YA KLABU au TIMU** ni muongozo mkuu unaobeba taratibu zote za uendeshaji wa Timu au Klabu na hivyo kuzingatiwa kama Sheria Kuu ya Timu au Klabu husika.
v) **KAMATI YA UTENDAJI:** Sekretariati ya Chama cha Mpira wa Kikapu XXXXXX
vi) **KURUGENZI**: vitengo vidogo vianvyosimamia maeneo ya ufanisi katika Chama.
vii) **KIONGOZI/VIONGOZI** ni mtu au watu waliochaguliwa miongoni mwa wajumbe mwenye karama ya kusimamia malengo au madhumuni ya wajumbe na kuwawezesha kufikia malengo waliojiwekea.
viii) **MSAJILI**: Msajili wa vilabu na vyama vya michezo
ii) **MICHEZO** ni shughuli au jambo linalofanywa na mtu, watu au kikundi wenye lengo la kushindana/kushindanishwa kwa ajili ya furaha au kupata tuzo fulani.
iii) **MJUMBE/WAJUMBE** ina maana mtu au watu ambao ni wanachama wa klabu au Timu ya michezo
iv) **TBF**: Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (Tanzania Basketball Federation)
v) **TIMU au KLABU** ni kundi la msingi la awali lililo jikusanya na kujisajili kwa madhumuni ya kucheza mpira wa Kikapu
vi) **SHIRIKISHO** Maana yake ni Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF)
vii) **MIKOA** Kiutawala ni wanachama na msingi katika shirikisho.
viii) **FIBA**: Shirikisho la Mchezo wa Kikapu Ulimwenguni (Federation Internationale de Basketball)
ix) **WAZIRI**: Maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya kushughulikia michezo

### IBARA YA 5

### A: MADHUMUNI YA KUUNDA CHAMA

**YYYYY** itajishughulisha na kusimamia, kuongoza, kuhamasisha, kukuza na kuendeleza masuala yote yanayohusu mchezo wa Mpira wa Kikapu katika Mkoa wa XXXXX kwa kutekeleza yafuatayo:-

i) Kuongoza na kusimamia shughuli zote za Mchezo wa Mpira wa Kikapu ndani ya Mkoa wa XXXXX.

ii) Kujenga ushirikiano na upendo kwa wakazi wa XXXXX kupitia shughuli za Mchezo wa Mpira wa Kikapu.
iii) Kushiriki na kuratibu Mashindano ya Mchezo wa Mpira wa Kikapu yanayofanyika katika maeneo mbalimbali ndani ya Mkoa wa XXXXX.
iv) Kuunda na kuandaa ushiriki wa Timu ya Mkoa wa XXXXX au Timu nyingine katika mashindano ya Kitaifa na Kimataifa.
v) Kubuni, kukuza, kuendeleza na kutekeleza programu za kiufundi na maendeleo ya mchezo wa Mpira wa kikapu katika Mkoa wa XXXXX
vi) Kuandaa na kuratibu mpango wa upatikanaji wa vyanzo vya fedha na vifaa pamoja na ujenzi wa viwanja vya mchezo wa mpira wa kikapu
vii) Kudhibiti na kusimamia uteuzi wa walimu, waamuzi na wakufunzi wa mpira wa kikapu katika Mkoa wa XXXXX.
viii) Kutoa elimu ya afya bora kwa vijana kupitia michezo ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na vitendo viovu kwa jamii.
ix) Kushirikiana na mikoa mingine katika uratibu na uendelezaji wa Mpira wa kikapu Nchini.
x) Kusimamia usajili wa wachezaji, makocha, wakufunzi na waamuzi wa Mchezo wa Mpira wa kikapu.
xi) Kusimamia ustawi wa Timu/Klabu katika vitongoji, wilaya na Mkoa
xii) Kufanya jambo lolote muhimu kwa manufaa ya maendeleo ya mpira wa kikapu.
xiii) Kuzingatia sheria Na:12 ya Baraza la Michezo Tanzania ya Mwaka 1967; Kanuni za usajili ya Mwaka 1999; Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995, na Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997.
xiv) Itashirikiana na Serikali, Taasisi za Serikali, Watu Binafsi pamoja na Mashirika yanayotoa elimu ya uhamasishaji wa jamii kujitambua ili kuthamini utaifa na kudumisha uzalendo kupitia michezo.

## SURA YA PILI

### IBARA 6
### UANACHAMA

i) Kutakuwa na aina tatu za uanachama yaani Mwanachama wa Msingi, Mwanachama wa Kushirikisha na Mwanachama wa Heshima
ii) Timu au Klabu ambazo zimejisajili kushiriki katika Mchezo wa kikapu katika Mkoa wa XXXXX itakuwa ndiye Mwanachama wa Msingi wa YYYYY
iii) Vyama vyote vinavyohusu masuala ya Mpira wa Kikapu kwa upande wa Makocha, Waamuzi, wataalamu, mambo mengine au Asasi za michezo basi watakuwa ni Wanachama Washiriki wa YYYYY na watatakiwa kutuma maombi ya uanachama
iv) Mtu, Watu, taasisi au Chama cha Hiari kitakachokuwa kimetoa mchango mkubwa katika kuendeleza Mchezo wa Mpira wa Kikapu Mkoa wa XXXXX basi watapewa uanachama wa Heshima wa YYYYY.
v) Kila Mwanachama ataheshimu na kukubaliana na masharti ya Katiba ya Chama na kutekeleza sheria, kanuni, na maamuzi yote ya YYYYY.
vi) Kila mwanachama anatakiwa alipe ada ya kiingilio pamoja na ada ya kila mwaka ya uanachama wa YYYYY kama ilivyopangwa na kukubalika na wanachama
vii) Kila Timu/Klabu itatakiwa kujisajili chini ya sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya 1971 ya BMT, pamoja na kanuni zake Na. 442 za mwaka 1999 na kuwasilisha nakala ya cheti cha usajili.
viii) Kila mwanachama atashiriki katika shughuli mbalimbali na vikao vitakavyoandaliwa na uongozi wa YYYYY kwa mujibu wa masharti yatakayoainishwa kwenye katiba hii.
ix) Maombi ya uanachama yakikataliwa kwa sababu zozote; Katibu Mkuu atamjulisaha aliyekataliwa maombi yake na kumjulisha sababu za kukataa ombi lake pamoja na kurudisha ada yake.

**IBARA YA 7**

**KIINGILIO NA ADA YA UANACHAMA**

i) Kila anayetaka kuwa mwanachama atatuma maombi yakiambatana na kiingilio na ada ya Uanachama kabla ya kukubaliwa.

ii) Kutakuwa na kiingilio kwa mwanachama mpya na ada ya kila mwaka. Viwango vya ada na viingilio vitapangwa na Kamati ya Utendaji. Viwango hivi vinaweza kubadilika kutokana na mabadiliko ya wakati

**IBARA YA 8**

**HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA**

i) Mwanachama atakuwa na haki ya kushiriki mikutano na vikao vya Chama vinavyomhusu na pia kutoa mawazo au maoni yake kwa kadiri inavyofaa bila kuvunja masharti ya Katiba hii.

ii) Mwanachama atakuwa na haki ya kuchagua viongozi wa Chama kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

iii) Mwanachama atakuwa na haki ya kugombea uongozi wa ngazi yeyote ndani ya Chama kulingana na taratibu za uongozi wa Chama zilivyoanishwa au zitakazopendekezwa.

iv) Mwanachama atashiriki mashindano yanayoandaliwa na Chama yanayomhusu

v) Mwanachama atakuwa na haki ya kujitetea endapo atatuhumiwa kwa kosa lolote.

vi) Atakata rufaa kuhusu jambo lolote linaloamliwa dhidi yake kwenye Kamati Kuu ya Utendaji ya Chama na kama hataridhika atakata rufaa kwa Afisa Michezo wa Mkoa kwa masahauriano zaidi.

vii) Mwanachama atakuwa na wajibu wa kutii na kufuata sheria na kanuni zote za Chama.

viii) Atakuwa na wajibu wa kujitolea kwa hali na mali kutetea na kulinda maslahi ya Chama pamoja na kutii uongozi uliopo madarakani

**IBARA YA 9**

**UKOMO NA KUPOTEZA UANACHAMA**

Mwanachama kama alivyotajwa katika **IBARA YA 6** ya Katiba hii, atapoteza uanachama iwapo:-

i) Atasimamishwa na kufutwa na Msajili wa Vyama vya Michezo kwa mujibu wa Sheria za BMT

ii) Atakiuka kwa makusudi Katiba ya YYYYY kwa kiasi cha kuathiri uongozi, usimamizi na maendeleo ya Mchezo wa Mpira wa Kikapu katika Mkoa wa XXXXX.

iii) Ataomba kujiuzuru au kufutwa uanachama

iv) Atashindwa kulipa ada ya kiingilio pamoja na ada ya uanachama katika muda uliopangwa kwa vipindi viwili mfululizo

v) Atashindwa kushiriki katika shughuli mbalimbali zilizoandaliwa na Chama cha Mpira wa Kikapu XXXXX kwa muda wa vipindi vitatu mfululizo bila kutoa taarifa maalum.

vi) Ataachishwa uanachama kwa kosa lolote baada ya kuonywa zaidi ya mara tatu juu ya vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu dhidi ya Chama au mamlaka ya Uongozi

vii) Endapo Mwanachama ameamua kujitoa kwa hiari yake mwenyewe, basi YYYYY haitawajibika kumrudishia mali, ada au michango yake yoyote aliyotoa hapo awali.

**IBARA YA 10**

**KURUDISHIWA UANACHAMA**

Mwanachama aliyepoteza uanachama anaweza kurejeshwa tena uanachama wake iwapo:-

i) Ataomba kwa maandishi kurejeshwa katika Chama ikiwa pamoja na kukubaliana na masharti ya Katiba hii

ii) Atalipa ada yote ya kiingilio na uanachama aliyokuwa anadaiwa hapo awali na pindi alipoachishwa

iii) Atakiri na kuomba msamaha kwa maandishi kutokana na makosa ya kutoshiriki katika shughuli mbalimbali zilizoandaliwa na Chama

iv) Mwanachama aliyeachishwa kwa kosa la wizi, ubadhilifu au ufujaji wa mali za Chama hatapewa msamaha wowote na atashitakiwa kulingana na kosa lake

# SURA YA TATU

## IBARA YA 11

## MUUNDO WA UONGOZI, SIFA, KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA CHAMA

**A: AINA ZA UONGOZI**

i) Mwenyekiti
ii) Makamu Mwenyekiti
iii) Katibu Mkuu
iv) Katibu Mkuu Msaidizi
v) Mwekahazina
vi) Kurugenzi Tisa za uendeshaji
vii) Walezi wa Chama

**B. SIFA YA KIONGOZI**

Wagombea wa Chama cha Mpira wa Kikapu XXXXX wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo

- Awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 25 kwa ajili ya kugombea nafasi za uongozi. Aidha, kwa upande wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wawe na umri usiopungua miaka 30
- Awe na akili timamu, mwenye shughuli au kazi inayoeleweka
- Awe mwaminifu, mwadilifu na mwenye tabia nzuri kwa jamii
- Awe na elimu ya Chuo na kuendelea na anayeonyesha kufanikiwa katika uongozi
- Awe na uzoefu na ujuzi wa kitaifa au kimataifa katika masuala ya usimamizi wa michezo na nafasi anayoomba
- Awe mwenye hekima, busara na mwenye moyo wa kujitolea kufanya majukumu ya Chama
- Awe tayari kupokea ushauri kwa maslahi ya kuendeleza Mchezo wa Mpira wa Kikapu.
- Awe na ufahamu juu ya Chama na Taasisi zake, ajue shughuli zake na uendeshaji.
- Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika lugha ya kiswhilil na kiingereza ambazo zinatumiwa na Chama.
- Awe hajapatikana na hatia ya kosa lolote la jinai hususani linalogusa na kushusha hadhi, utu na haiba mbele ya jamii (kama wizi, mauaji, kubaka, madawa ya kulevya n.k.)
- Awe amewahi kuwa mchezaji wa mpira wa kikapu, au kuhudhuria mafunzo ya ualimu wa mpira wa kikapu, uamuzi, utawala wa michezo, tiba ya wanamichezo, au utunzaji na utengenezaji wa viwanja vya michezo.

## IBARA YA 12

## MUDA WA UONGOZI

i) Kipindi cha uongozi wa shirikisho ni miaka minne (4). Kiongozi yoyote wa YYYYY anaweza kuchaguliwa kuongoza kwa vipindi vingine bila kuwa na mpaka wa uongozi.
ii) Kiongozi ambae atajiuzulu uongozi katika nafasi fulani baada ya kuitumikia kwa zaidi ya miaka mitatu atahesabika kuwa ametumikia kipindi kizima.
iii) Endapo kutatokea nafasi ya wazi ya uongozi kutokana na sababu yoyote, nafasi hiyo itajazwa na mamlaka zenye dhamana hiyo kwa mujibu wa katiba hii katika kikao kinachofuata.

## IBARA YA 13

## KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA CHAMA

**1. Mwenyekiti wa Chama :**

i) Atakuwa Kiongozi Mkuu wa Chama mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa madhumuni ya Chama.
ii) Atakuwa Mwenyekiti wa Mikutano yote ya Chama.

iii) Atahusika katika kutafuta vyanzo vya mapato, kusimamia matumizi ya fedha pamoja na kuidhinisha malipo ya Chama.
iv) Atahakikisha kuwa shughuli zote za kila siku za Chama zinaendeshwa kwa mujibu wa Katiba kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na ufanisi wa kazi.
v) Atafuatilia kuona kuwa maagizo yote yatokanayo na Kamati ya Utendaji au ushauri unaotolewa na wajumbe pamoja na vyombo vya juu vya mamlaka vinatekelezwa ipasavyo.
vi) Kwa kushirikiana na Katibu wataitisha vikao vyote vya Chama kwa mujibu wa Katiba au pale anapoona inafaa kufanya hivyo.
vii) Atakuwa mwakilishi wa Chama kwenye vyombo vingine vya michezo kutegemeana na Katiba za vyombo hivyo au kwenye vikao vingine kwa mujibu wa nafasi yake.
viii) Atasimamia na kuongoza Kamati Kuu, Kamati ya Utendaji ya Chama pamoja kutoa maelekezo kwa maendeleo ya Chama.
ix) Atakuwa na kura ya ziada ya uamuzi endapo kunatokea sare ya kura, isipokuwa kwa suala la uchaguzi.
x) Atawajibika kulinda na kuitetea kwa nguvu zake zote Katiba ya Chama.
xi) Atakuwa msimamizi na Mdhibiti Mkuu wa shughuli na maendeleo ya watumishi wote walioajiriwa na Chama.
xii) Anaweza kushiriki katika kikao chochote cha shirikisho kwenye ngazi ya chini.

**2. Makamu Mwenyekiti wa Chama**

i) Atakuwa na kazi na madaraka yote ya Mwenyekiti kama yalivyoainishwa katika aya ya 1 ya ibara hii iwapo Mwenyekiti hayupo.
ii) Ataongoza vikao kwa niaba ya Mwenyekiti ikiwa hatakuwepo.
iii) Atakuwa msaidizi wa Mwenyekiti katika majukumu yote yanayohusu Mwenyekiti.
iv) Atafanya kazi atakazo elekezwa na Mwenyekiti wa Chama, Kamati ya Utendaji na Mkutano mkuu wa Chama.
v) Atajishughulisha na ustawi wa Mpira wa Kikapu na kuhamasisha kujiunga kwa wanachama wapya.
vi) Atamwakilisha Mwenyekiti katika vikao ambavyo hayupo pamoja na kufanya kazi atakazoelekezwa naye

**3. Katibu Mkuu wa Chama**

i) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa shughuli za kila siku za Chama na atafanya kazi chini ya Mwenyekiti na Kamati ya Utendaji.
ii) Ataratibu vikao vyote vya Chama kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za Katiba**.**
iii) Atasimamia mipango yote ya Chama pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Chama.
iv) Ataandaa taarifa, mihtasari na machapisho mengine yanayohusu Chama na kuyawasilisha kwenye Kamati ya Utendaji, Mkutano Mkuu wa Chama wa mwaka au mkutano wowote wa Chama pindi anavyotakiwa kufanya hivyo.
v) Atakuwa mwandishi katika mikutano na kuweka kumbukumbu zote za Chama.
vi) Ataandaa taarifa ya kazi za maendeleo ya Chama ya robo mwaka,nusu mwaka na mwaka pamoja na kalenda ya kazi na kuiwasilisha kwenye vikao vya Chama, Mikutano ya wanachama, Afisa Michezo wa Mkoa, Kamati ya michezo ya Mkoa na msajili wa michezo Mkoa.
vii) Ataandaa bajeti, Mpango kazi na Mpango wa utekelezaji wa shughuli zote za Chama.
viii) Atafanya kazi nyingine kadiri atakavyoelekezwa na Mwenyekiti na Kamati ya Utendaji

**4. Katibu Msaidizi wa Chama**

i) Atakuwa msaidizi wa Katibu katika majukumu yote yanayohusu Katibu Mkuu wa Chama.
ii) Atafanya kazi atakazo elekezwa na Mwenyekiti wa Chama, Katibu wa Chama, Kamati ya Utendaji na Mkutano Mkuu wa Chama.

iii). Atafanya kazi nyingine zozote atakazoelekezwa na Mwenyekiti au Katibu

**5. Mwekahazina wa Chama**

i) Atakuwa Mshauri Mkuu wa Chama kwa masuala yahusuyo fedha na usimamizi wake.

ii) Atapokea fedha na kukusanya mapato ya Chama na kukatia risti kwa kila fedha anayoipokea au kukusanya.

ii) Atatunza mapato yote ya Chama kwa njia iliyoidhinishwa na Chama kufuatana na Katiba hii na kuweka kumbukumbu sahihi za mapato na matumizi.

iv) Atabuni na kuandaa mipango ya upatikanaji wa fedha za Chama.

v) Ataandaa makisio ya Mapato na Matumizi na pia taarifa za Mapato na Matumizi ya kila mwaka na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Utendaji na Mkutano Mkuu wa Chama.

vi) Atakuwa mmojawapo wa viongozi waliochaguliwa kutia saini ya masuala ya fedha.

vii) Ataandaa taarifa zote zinazohusu masuala ya fedha na kuziwasilisha kwa Mwenyekiti, Katibu na mamlaka husika

viii) Atatunza fedha na vitabu vya hesabu na nyaraka zote zinazohusu masuala ya fedha.

**6. Kurugenzi Tisa za Uendeshaji**

Kutakuwa na kurugenzi Tisa za Uendeshaji ambazo viongozi wake watachaguliwa na Kamati Kuu miongoni mwa Wanachama kulingana na ushiriki na ubora wao katika kusimamia na kuendeleza mpira wa Kikapu Mkoa wa XXXXX. Kurugenzi hizo ni

i) Kurugenzi ya Ufundi na Mashindano

ii) Kurugenzi ya Mipango na Maendeleo

iii) Kurugenzi ya Watoto na Maendeleo Vijana

iv) Kurugenzi ya Wanawake

v) Kurugenzi ya Watu wenye Ulemavu

vi) Kurugenzi ya Makocha

vii) Kurugenzi ya Waamuzi

viii) Kurugenzi Afya na Tiba michezoni.

ix) Kurugenzi ya Katiba, Sheria na Maadili

- Utekelezaji wa majukumu ya kila Kurugenzi yatasimamiwa na Kanuni zitakazokuwa zimetungwa na kila kurugenzi husika bila kuathiri Katiba hii. Aidha wakurugenzi wote watahusika na utawala wa shughuli za Kurugenzi wanazosimamia.
- Watakuwa sehemu ya kamati ya Utendaji wa Chama pamoja na kuwa washauri wakuu wa maeneo wanayoyasimia

**7. Mlezi wa Chama**

- Kutakuwepo na Mlezi atakayeteuliwa Kamati Kuu na kuthibitishwa na Kamati ya utendaji na kutolewa taarifa katika Mkutano Mkuu wa Chama.
- Mlezi atakuwa mshauri mkuu wa mambo yote ya maendeleo ya mpira wa kikapu
- Mlezi atashika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne lakini anaweza kuchaguliwa tena.
- Mlezi anaweza kuhudhuria kikao chochote cha Chama katika ngazi yoyote.

# SURA YA NNE

## IBARA YA 14

## MIKUTANO MBALIMBALI YA CHAMA CHA MPIRA WA KIKAPU

Kutakuwa na aina ya Tano ya Mikutano kama ifuatavyo:-

- Mkutano Mkuu
- Mkutano Mkuu maalumu wa Chama
- Mkutano wa Kamati ya Utendaji
- Mkutano wa Uchaguzi Mkuu wa Chama

Taarifa zote za mikutano zitatolewa kwa wajumbe au wanachama wote kwa kutumia taratibu zozote za kutolea taarifa zinazokubalika. Taarifa hii itaonyesha, aina ya mkutano, tarehe ya mkutano,dhumuni, wahusika, muda na mahali panakofanyika mkutano.

**A. KAZI ZA MKUTANO MKUU WA CHAMA**

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Chama ambao utakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Mkutano Mkuu wa Chama utakutana mara moja kwa mwaka ila unaweza kuitwa kwa dharula baada ya Mwenyekiti kushauriana na Kamati Utendaji.
ii) Mkutano Mkuu wa Chama utapitia na kupewa taarifa kuhusu maendeleo ya chama na utatoa maoni, mapendekezo na ushauri kwa Kamati ya Utendaji
iii) Mkutano Mkuu wa Chama unaweza kupiga kura ya kutokuwa na imani na kiongozi wa Chama baada ya kushauriana na Kamati Kuu na kuridhiwa kufanya hivyo
iv) Mkutano Mkuu wa Chama utaitishwa na Mwenyekiti akishauriana na Katibu Mkuu na pia unaweza kuitishwa na Msajili Msaidizi wa vyama vya michezo Wilaya/Mkoa.
v) Mkutano Mkuu utapokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka Kamati ya Utendaji ya Chama, Kamati Ndogo au Kurugenzi kuhusu maendeleo mbalimbali ya Mpira wa Kikapu
vi) Mkutano Mkuu wa Chama utatoa maoni, mapendekezo na ushauri kuhusu maamuzi yoyote yanayohusu Chama ili yaridhiwe kwa utekelezaji.
vii) Mkutano Mkuu wa Chama utahudhuliwa na Wanachama wote halali na utakuwa na baraka ya kutoa maamuzi ikiwa akidi itafika theluthi mbili waliohudhuria Mkutano husika
viii) Taarifa ya Mkutano mkuu sharti itolewe kwa maandishi kwa wajumbe sio chini ya mwezi mmoja kabla ya tarehe ya kikao.
ix) Mkutano Mkuu wa mwisho wa Chama wa kipindi cha miaka Minne (4) utafanyika kabla ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi siku 30 kabla ya uchaguzi. Na utakabidhi madaraka kwa Kamati ya Uchaguzi itakayokuwa na wajumbe Sita (6) ambao watatu watachaguliwa na Mwenyekiti na wawili (2) watachaguliwa na msimamizi wa uchaguzi
x) Idadi ya wajumbe kwenye mkutano Mkuu sharti isipungue zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wenye haki ya kupiga kura.
xi) Endapo idadi ya wajumbe waliohudhuria haifikii kiwango zaidi ya nusu, mkutano utahairishwa kwa muda usiopungua siku 30.

**B: KAZI ZA MKUTANO MKUU MAALUM WA CHAMA**

Kutakuwa na Mkutano Mkuu Maalum wa Chama ambao utakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama utaitishwa na Katibu Mkuu kwa maelekezo ya Mwenyekiti, Kamati Kuu au Kamati ya Utendaji baada ya kushauriana wajumbe
ii) Utajadili jambo la maalum au la dharura ambalo linamuonekano wa kuathiri utendaji kazi wa Chama au linahitaji maamuzi ya haraka kwa faida ya maendeleo ya Mpira wa Kikapu wa Mkoa wa XXXXX
iii) Ajenda ya Mkutano Mkuu Maalum wa Chama lazima iwasilishwe kwenye Kamati Kuu siku Saba (7) kabla ya kuitishwa kwa Mkutano husika.

**C: KAZI ZA MKUTANO MKUU WA KAMATI YA UTENDAJI**

i) Kamati ya Utendaji kitakuwa ni chombo cha watendaji wakuu wa kazi za kila siku za Chama na itakuwa ndiyo Sekretarieti ya YYYYY.
ii) Kamati ya Utendaji itakutana mara moja kila baada ya miezi miwili.

iii) Kikao cha kamati ya Utendaji kitaitishwa na Katibu baada ya kushauriana na Mwenyekiti kufanya hivyo.
iv) Taarifa ya maandishi ya kikao cha kamati, sharti itolewe siku Kumi (10) kabla ya kikao cha kamati.
v) Kiwango cha wajumbe kwenye kikao cha kamati, kitakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote.
vi) Mwenyekiti ndiye ataongoza kikao cha Kamati ya Utendaji akisaidiwa na Katibu Mkuu.
vii) Endapo akidi haitimii, au Mwenyekiti na Katibu hawatafika kwa sababu yoyote ile baada ya kuitisha kikao, kikao kitaahirishwa kwa muda usiopungua siku saba.
viii) Kubuni na kupanga mbinu na utekelezaji wa maagizo ya Kamati Kuu pamoja na wanachama.
ix) Kuhakiki na kufanya mapitio ya kanuni za uendeshaji wa mashindano mbalimbali ya mpira wa Kikapu katika Mkoa.
x) Kuratibu masuala yanayohusu mpiwa wa kikapu kwa wachezaji, makocha na waalimu.
xi) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa kurugenzi zilizoainishwa kwenye Katiba hii.
xii) Kujadili na kushughulikia taarifa za utekelezaji wa kazi za kila siku za Chama ikiwa ni pamoja na taarifa za mapato na matumizi ya kila robo mwaka.
xiii) Itashiriki katika kuandaa Bajeti ya Chama, Mpango kazi wa Chama na Mpango wa Utekelezaji wa Chama.
xiv) Kupokea, kujadili na kutoa uamuzi juu ya malalamiko na rufaa kadri zitakavyowasilishwa.
xv) Kuhakikisha kuwa Katiba, Kanuni na taratibu za mchezo wa Mpira wa Kikapu zinafuatwa na kuzingatiwa.

**D. KAZI ZA MKUTANO WA UCHAGUZI MKUU WA CHAMA**

Kutakuwa na Mkutano Mkuu Maalum wa Uchaguzi ambao utakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Uchaguzi utakaohusika kuchagua viongozi wa Chama kwa mujibu wa Sura ya Tatu; Ibara ya 11 ya Katiba hii.
ii) Mkutano Mkuu wa uchaguzi utasimamiwa na Kamati ya Michezo ya Wilaya/Mkoa, Idara ya Michezo na Utamaduni na Baraza la Michezo la Wilaya/Mkoa.
iii) Mgombea yeyote wa uchaguzi atajaza fomu ya maelezo binafsi itakayotolewa na Idara ya Michezo na Utamaduni Wilaya/Mkoa (BMW). Wagombea wote watahojiwa na kupitisha majina ya wagombea ambayo yatafikishwa mbele ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi na kupigiwa kura.
iv) Upigaji wa kura utafanyika kwa kupiga **KURA ZA SIRI** na utahusisha wajumbe wafuatao; Mwenyekiti na Katibu wa Timu/Klabu pamoja na Mchezaji mwakilishi mmoja kutoka kila Timu/ Klabu
v) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji hawatakuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi kwa vyeo vyao.
vi) Wanachama wote ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi.
vii) Wajumbe wa mkutano Mkuu wa Uchaguzi ni wale tu ambao timu zao zimesajiliwa na hazidaiwi ada ya mwaka.

## SURA YA TANO

### IBARA YA 15

### VYANZO VYA MAPATO, UTUNZAJI NA MATUMIZI YA FEDHA YA CHAMA

**A: Vyanzo vya mapato vya Chama vitakuwa ni:-**

i) Ada ya kiingilio na michango ya wanachama
ii) Michango midogomidogo kutokana na harambee
iii) Misaada ya wafadhili kutoka kwa wahisani, wafadhili na walezi
iv) Miradi na uwekezaji kwenye vitega uchumi vya Chama
v) Mauzo na mali au faida kutoka katika miradi mbalimbali itakayowekezwa na Chama
vi) Mapato kutoka kwenye michezo na matamasha ya kutunisha Mfuko wa Chama

**B: Utunzaji na Matumizi ya Fedha ya Chama itakuwa kama ifuatavyo:-**

i) Mfuko wa kutunzia fedha itakuwa Benki inayotambuliwa na kukubaliwa na Wanachama na fedha zote zitatunzwa Benki
ii) Waweka saini katika akaunti inayotambuliwa na Klabu hawatazidi wanne
iii) Namna bora ya kutoa/kuweka fedha itazingatia sheria na kanuni za Benki husika
iv) Mwenyekiti, Katibu na Mwekahazina watahusika katika ukusanyaji wa michango midogomidogo ya wadau wa mchezo huu pamoja na utunzaji wa mali za Chama
v) Matumizi yoyote ya Chama yatatumika kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa, mahitaji ya Mpango Mkakati na Mpango Kazi uliopendekezwa kutekelezwa.
vi) Mwenyekiti ataridhia matumizi ya fedha za chama kulingana na bajeti, Mpango Mkakati na Mpango Kazi

# SURA YA SITA

## IBARA YA 16

## KUTOFANYIKA KWA UCHAGUZI, MIGOGORO, MAREKEBISHO YA KATIBA, AKIDI, KUVUNJIKA KWA CHAMA

**A: KUTOFANYIKA KWA UCHAGUZI**

Uchaguzi uliopangwa ukishindikana kufanyika kwa sababu yoyote ile, uongozi uliopo madarakani utaendelea kukasimu madaraka ya kuongoza hadi hapo uchaguzi mwingine utakapopangwa na viongozi wapya kupatikana.

**B: MIGOGORO**

- Hairusiwa kwa mtu, chombo, klabu au shirikisho kufikisha suala la mgogoro wowote dhidi ya YYYYY katika mahakama, isipokuwa kwa masuala ya ubadhilifu au wizi wa fedha au mali za Chama.
- Migogoro katika Chama itatuliwa kwa kuzingatia Katiba hii pamoja na Sheria na Kanuni za Baraza la Michezo la Taifa (BMT).
- Mtu, Timu, au chombo chochote kitakachokiuka masharti ya Katiba hii atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria na kanuni za Baraza la Michezo la Taifa (BMT)

**C: MAREKEBISHO YA KATIBA**

Marekebisho yoyote ya Katiba hii yatafanywa kwa uamuzi wa wajumbe wasiopungua theluthi mbili ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu waliohudhuria na wenye haki ya kupiga kura. Mambo yoyote yatakayojitokeza ambayo hayakuelezwa katika Katiba hii yataamuliwa na mamlaka zinazosimamia michezo katika Mkoa wa XXXXX.

**D: AKIDI**

Akidi ya Maamuzi kwenye Mikutano yote ya Chama iliyotambuliwa kwenye **IBARA YA 14** itakuwa theluthi mbili ya wajumbe

**E: MIKATABA**

Chama cha Mpira wa Kikapu XXXXX (YYYYY) kitakuwa huru kuwekeana mikataba na Wadau mbalimbali kwa mujibu wa sheria za Serikali. Pamoja na Mikataba hii, Chama kitaweka Mikataba ya kisheria kwa muda mfupi au mrefu kwa maandishi kulingana na malengo ya Chama chini ya Mwanasheria wa Chama.

**F: KUVUNJIKA KWA CHAMA**

Iwapo kutatokea migogoro yoyote itakayopelekea Chama kuvunjika, basi kulingana na taratibu za kisheria malipo ya madeni na madai yatafanyika na iwapo hapatakuwa na madeni, basi mali za Chama zilizopo kwa mujibu wa sheria zitauzwa ili kufidia malipo ya madeni au madai yaliyowasilishwa.

**G: KUKIRI**

Katiba hii imetungwa chini ya sheria namba 12 ya mwaka 1967 ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na marekebisho yake ya sheria namba 6 ya mwaka 1971. Hivyo Katiba hii inazingatia Sheria na Kanuni za Baraza la Michezo la Taifa.

| | |
|---|---|
| …………………………………… | …………………………………………… |
| **MAJINA KAMILI YA MWENYEKITI** | **MAJINA KAMILI YA KATIBU** |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**TAREHE DD DESEMBA 2021**